HAKI ZANGU

NA

MAHAKAMA YA KIMATAIFA

DHIDI YA UHALIFU

NIKIWA MWANAMKE MKENYA

FEDERATION OF WOMEN LAWYERS

HAKI ZA AKINA MAMA

FIDA KENYA

Shukrani

Nakala hii ya *Haki Zangu na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu* imetayarishwa na kuchapishwa na Chama cha Mawakili Wanawake Kenya (FIDA). Tunamshukuru Dk. Elizabeth W. Muli ambaye alitayarisha nakala hii iliyorahisishwa. Pia tungependa kumshukuru Mkurugenzi Mkuu, Grace Maingi Kimani, Mkurugenzi Msaidizi na Mkuu wa Miradi, Claris Ogangah na wafanyakazi wenzetu, Judith Okal na Anne Buluma ambao walihariri jarida hili.

Shukrani za dhati ziende kwa OPEN SOCIETY INSTITUTE – OSI kwa kutoa msaada wa kifedha wa kuweka pamoja na kukusanya na kuchapisha jarida hili.

FIDA Kenya inatumaini jarida hili litakuwa na manufaa kwa wanawake wa Kenya wa rika zote, wakitumia nafasi hii kutambua ukiukaji wa haki zao na kutoa sauti zao zisikike na Mahakama ya Kimataifa Dhidi ya Uhalifu (ICC).

Grace Maingi Kimani

Mkurugenzi Mkuu

FIDA KENYA

Utangulizi

Tume ya Uchunguzi ya Vurugu zilizofuatia Uchaguzi Mkuu uliopita (CIPEV) ambayo ilikuwa iundwe mnamo tarehe 23 Mei, 2008 ilibainisha kwamba uhalifu dhidi ya binadamu ulitendeka Kenya. Ilifafanua kiwango na ukubwa wa uhalifu huu na athari zake kwa wanawake. Wanawake walinajisiwa, wakauawa, kuharibiwa mali na kuhamishwa kutoka makazi yao. Zaidi ya Wakenya 1,000 waliuawa na wengine 30,000 wakakosa makazi ya kuishi. CIPEV ilipendekeza kwamba watu wanaohusika zaidi na uhalifu huo washtakiwe kupitia Mahakama Maalum itakayoundwa Kenya. Iwapo Mahakama hiyo maalum haitaundwa, ikapendekezwa kwamba washukiwa washtakiwe katika Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu (ICC) huko The Hague.

Jitihada za kuunda Mahakama Maalum zilishindikana, kwani miswada kadha kuhusiana na kuundwa kwa mahakama hiyo ilikataliwa bungeni. Ukosefu wa kujitolea kisiasa kufikisha mahakamani uhalifu wa kutisha uliofanyika wakati wa vurugu zilizofuatia matokeo ya uchaguzi mkuu na hali hii inaendelea hadi leo. CIPEV iliwasilisha orodha ya washukiwa kwa Kamati ya Viongozi Maarufu Afrika iliyoongozwa na Bw. Kofi Annan ambaye aliwasilisha orodha hiyo kwa ICC. Mashirika kama vile Tume ya Kutetea Haki za Binadamu Kenya (KNCHR) pia yaliwasilisha taarifa iliyopewa jina la, “Katika kingo za jabali: Tathmini ya haki za binadamu katika vurugu zilizofuatia uchaguzi mkuu wa 2007 Kenya.”

Mnamo tarehe 31 Machi, 2010, kitengo cha mashtaka cha ICC kilimruhusu Mwendesha Mashtaka Louis Moreno Ocampo aanze upelelezi kuhusiana na uhalifu ambao ulifanyika Kenya wakati wa vurugu zilizofuatia uchaguzi mkuu kuanzia 2007-2008. Uamuzi huu ulikuwa mwanzo wa kile kilichotajwa kama “Hali ya Kenya,” ambayo ni mojawapo ya maswala yaliyopo mbele ya Mahakama ya Kimataifa dhidi

ya Uhalifu. Hatua hii ya ICC kupitia jitihada za Mwendesha Mashtaka ilichukuliwa kwa kuwa miaka miwili baada ya uhalifu kutendeka hakuna yeyote aliyeshtakiwa katika mahakama za Kenya.

Wakati Wakenya wanajua kwamba kuna ICC, ama inavyojulikana maarufu kama “The Hague” ambayo inaweza kuwashtaki wanaodaiwa kuhusika na uhalifu uliotajwa, wengi bado hawajui jinsi wanavyoweza kujihusisha na mahakama. Mahakama hiyo inafanyaje kazi? Je kesi zinazofikishwa kwenye mahakama hii zinashughulikiwa kama zile za mahakama za hapa nchini? Je muathirika anaweza kuwasilisha madai ya fidia na atafanyaje hivyo? Je, haki za wanawake zinalindwa na ICC? Haya ni baadhi ya maswali machache ambayo mwongozo wa nakala hii unatarajia kuyajibu.

Madhumuni ya chapisho hili ni kuleta uelewa kuhusu ICC na kuwahamasisha wanawake wajitayarishe kupata haki zao kupitia utaratibu mzima wa kesi kuanzia uchunguzi, usikilizaji wa kesi, hukumu na rufaa. Sheria ya Rome ambayo iliunda ICC inalenga zaidi kutambua mwathirika na kutambua mahitaji ya waathirika kusikilizwa, kushiriki na kupata haki. Inalinda haki za wanawake na waathirika kama washirika muhimu katika shughuli za mahakama.

Orodha ya Vifupisho

ICC	-	Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu
UNSC	-	Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa
DRC	-	Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo
RPE	-	Sheria za Utaratibu na Ushahidi
OPV	-	Afisi ya Umma ya Ushauri wa Waathirika
VPRS	-	Kitengo cha Ushiriki wa Waathirika na Utoaji Hukumu
VWU	-	Kitengo cha Waathirika na Mashahidi
GSU	-	General Service Unit
SGBV	-	Unyanyasaji wa ubakaji na aina nyingine za unyanyasaji wa jinsia
CIPEV	-	Tume ya Uchunguzi wa Vurugu za Baada ya Uchaguzi Mkuu
IDP's	-	Wakimbizi wa ndani ya Nchi
NGO's	-	Mashirika yasiyo ya Kiserikali

Yaliyomo

SURA 1 7

MFUMO NA JUKUMU LA ICC

SURA 2 17

HAKI YA WAATHIRIKA NA ICC

SURA 3 27

WANAWAKE NA ICC

SURA 1

MFUMO NA JUKUMU LA ICC

1. ICC ni nini?

Mahakama ya Kimataifa Dhidi ya Uhalifu (ICC) ni mahakama huru ya kudumu ambayo huwashtaki watu wanaotuhumiwa kufanya uhalifu wa kutisha unaogusa mataifa kama vile **mauaji ya halaiki**, **uhalifu dhidi ya binadamu** na **uhalifu wa kivita**. Ikiwa ni mahakama ya kudumu ya kimataifa, ICC ni tofauti na tume nyingine ambazo ziliundwa kufuatia matukio maalum na ambazo huwepo kwa muda uliopangwa. Makao Makuu ya Mahakama iko The Hague, Uholanzi.

ICC iliundwa na Mkataba wa Rome kuhusiana na Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu ambao ulipitishwa Rome, Italy mnamo Julai 17, 1998. Mkataba wa Rome ni wa kimataifa ambao unawajibisha nchi zote ambazo zilikubali kutii matakwa ya mkataba huu.

Hakikisho kwamba uhalifu wa kutisha zaidi uliojalisha jamii ya kimataifa kwa ujumla ni lazima uchukuliwe hatua za adhabu na kwamba kuendeshwa kwa kesi zake kwa ufanisi lazima kuhakikishwe kwa kuchukua hatua za kitaifa na kwa kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

Kupania kukomesha vitendo vya uhalifu bila kujali kwa wahusika wa uhalifu huu na hivyo kuchangia kuzuia uhalifu kama huo tena…

Kulingana na Mkataba wa Rome kwa ICC

Nchi hizi huwa ni washirika katika mkataba huu. Mkataba ulianza kutumika Julai 1, 2002, ambapo nchi 60 zilikuwa washirika. Kenya ilikuwa mshirika wa mkataba wa Rome wakati ilipotia sahihi mkataba huo mnamo Agosti 11, 1999 na kuipitisha kisheria mnamo Machi 15, 2005. Mnamo Desemba 12, 2008, Bunge lilipitisha sheria ya Kimataifa ya Uhalifu, 2008. Kwa hivyo Kenya inaweza kushtaki washukiwa wa uhalifu wa mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita katika mahakama zake. ICC pia inaweza kushtaki washukiwa wa uhalifu huu kama utatokea Kenya baada ya Machi, 2005 wakati Kenya ilipokuwa mshirika wa mkataba.

2. Kwa Nini Kuwe Na Mahakama Ya Kimataifa Dhidi Ya Uhalifu?

Katika karne iliyopita, uhalifu wa kutisha zaidi katika historia ya ubinadamu ulitendeka. Katika Afrika kulikuwa na mauaji ya halaiki nchini Rwanda mnamo mwaka 1994, kuanza kwa uhalifu mbaya zaidi ikiwemo kuingiza watoto vitani katika nchi za Sierra Leone na Uganda Kaskazini. Kuna migogoro inayoendelea na vitendo vya vurugu katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Darfur kati ya nyinginezo.

Wanawake na watoto ndio wamekuwa waathirika wakubwa zaidi hasa unyanyasaji wa kijinsia. Uhalifu huu umekuwa ukitendeka kwa muda mrefu, sababu wale wanaoandaa uhalifu huu hawajawahi kuwajibishwa na kuadhibiwa kwa sababu huenda wana madaraka makubwa. Waathirika wanaachwa bila usaidizi na wakijihisi wanyonge, bila ya uwezekano wa kutendewa haki.

ICC kwa kuwa ni mahakama ya kimataifa, haiko chini ya mamlaka ya nchi yoyote na inaweza kuwashtaki wahusika wa uhalifu wa kutisha bila ya kujali nyadhifa zao ama madaraka yao kisiasa. Inahakikisha kwamba hakuna sehemu ya kujificha kwa wale wanaotenda uhalifu wa kutisha na hakutakuwa na msamaha wa uhalifu wa kimataifa.

3. Wakati Gani ICC Inatumia Mamlaka Yake na Kuendesha Kesi?

Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu inasaidia mahakama ya kitaifa ili ziendelee kuwa na uwezo wa kushtaki mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu, uhalifu wa kivita na uhalifu wa ukandamizaji. Uwezo wa ICC unalenga kungoja ambapo inatoa kipaumbele kwa mahakama za kitaifa kuchunguza ama kushtaki. ICC haiwezi kushtaki uhalifu ambao ulitendeka kabla ya tarehe 1 Julai, 2002 wakati mkataba ulipoanza kutumika.

Kama kesi inashughulikiwa na nchi husika, ICC haiwezi kushtaki isipokuwa kama nchi hiyo haiko tayari ama haiwezi kuchunguza na kushtaki kwa haki.[1] Nchi inaweza kuonekana “haiko tayari” kama inaonekana wazi kumlinda mtu anayehusika na uhalifu unaohusika na ICC. Nchi inaweza kuonekana “haiwezi” wakati mfumo wake wa sheria hauna uwezo wa kushtaki kesi ama umeporomoka. Kwa sasa ICC ina kesi ambazo zimewasilishwa kwake na nchi shirika kama vile Uganda na DRC na UNSC kuhusiana na hali ya Darfur na waendesha mashtaka kuhusiana na Kenya.

ICC haiendeshi kesi zote ambazo zinahusisha uhalifu wa kutisha. Inaweza endesha zile ambazo zina uzito wa kutosha. Hii inamaanisha kwamba uhalifu unatakiwa uwe na uzito mkubwa na uwe umetendeka kwa kiwango ambacho kitagusa nchi za kimataifa.

[1] Art 17(1)(2) na (3) Mkataba wa Rome

4. ICC Huwa Inamshtaki Nani?

ICC hushtaki watu binafsi na sio makundi. Hakuna aliye huru dhidi ya mashtaka wakiwemo marais, viongozi wa siasa, wakuu wa jeshi ama mshukiwa yeyote, isipokuwa watu waliokuwa na umri chini ya miaka 18 wakati walipotenda uhalifu unaodaiwa kutendeka. Hata hivyo ICC haiwezi kumshtaki kila mhusika wa vurugu. Inalenga kushtaki na kuwawajibisha wale ambao wanahusika zaidi na uhalifu wa kutisha. Kinga cha mashtaka na sheria za kusamehe wakosaji sio utetezi unaokubalika mbele ya ICC.

5. Muundo Na Kazi za ICC ni Zipi?

Muundo wa ICC una vitengo vinne:

(i) **Urais** – Kuna majaji watatu (Rais mmoja na wasaidizi wawili) waliochaguliwa kutoka majaji 18 wa ICC. Kazi yao kuu ni usimamizi wa vitengo vya mahakama isipokuwa ofisi ya Mwendesha Mashtaka.[2]

(ii) **Mahakama** – Ina majaji 18 kutoka sehemu mbalimbali duniani kuangalia msingi wa kimataifa wa mahakama. Majaji wanachaguliwa na baraza la nchi shirika kulingana na uzoefu na ujuzi wao wa sheria za uhalifu na utaratibu, sheria ya kimataifa, sheria ya haki za binadamu na pia kama ni watu waaminifu, waadilifu na wasiokuwa na upendeleo. Jukumu lao ni kuhakikisha haki inatolewa bila upendeleo. Jaji Joyce Aluoch kutoka Kenya aliteuliwa kuanzia Mach i 11, 2009 kwa muda wa miaka tisa. Amepangiwa kitengo cha mashtaka. Kitengo hiki kina idara tatu ambazo ni:

[2] Art 38(1) na (2) Mkataba wa Rome

(a) **Kitengo cha Kabla ya Mashtaka (PTC)** – Majaji katika kitengo hiki wanasimamia jinsi mwendesha mashtaka anavyoendesha upelelezi na mashtaka. Pia wanahakikisha haki za washukiwa, waathirika na mashahidi zinalindwa wakati wa upepelezi. PTC inaamua iwapo kesi inafaa ama haifai kuendeshwa, iwapo hati za kukamatwa washukiwa ama kuitwa mahakamani mbele ya mwendesha mashtaka kama ilivyotakiwa na kuhakikisha mashtaka dhidi ya washukiwa. Pia mahakama inaamua kuhusu hali halisi ya kesi na kuamua iwapo waathirika wanaweza kushiriki katika mwenendo wa kesi.

(b) **Chumba cha Mashtaka** – Huendesha kesi mara baada mashtaka na kukamatwa kwa wadaiwa kuthibitishwa na kitengo cha kabla ya mashtaka. Majukumu yake makuu ni kuhakikisha kwamba mashtaka yanaendeshwa haraka na kwa usawa, kwa kujali haki za washukiwa pamoja na kuwalinda mashahidi na waathirika ambao wanaruhusiwa kushiriki, kutia hatiani au kuwaondolea mashtaka washukiwa, kuamua kutoa hukumu aidha kifungo, kulipa fidia au marekebisho ya tabia. Mahakama haitoi hukumu ya kifo.

(c) **Kitengo cha rufaa** – Husikiliza rufaa kutoka upande wowote kuhusiana na maamuzi kabla ya au wakati wa mashtaka. Kinaweza kubatilisha maamuzi ya mwisho ya kifungo, hukumu, kuendelea na kurekebisha ama kubadili rufaa na kutoa amri ya kesi kusikizwa upya.

(iii) **Ofisi ya Mwendesha Mashtaka**

– Hiki ni kitengo huru cha mahakama ambacho madhumuni yake ni kupokea na kutathmini maelezo yanayotolewa kwake kuhusiana na madai ya uhalifu ili kujua iwapo kuna sababu yeyote ya msingi ya kufanya uchunguzi kwenye uhalifu huo na kuwafikisha mahakamani wale wanaodaiwa kuhusika na uhalifu huo.

Louis Moreno Ocampo – Mwendesha Mashtaka

(iv) **Masijala** – Idara ya usajili inaongozwa na msajili na msaidizi wake na kazi yake kuu ni kutoa msaada wa kiutawala na kimahakama wa vitengo vyote vya mahakama na hasa kusaidia mahakama kuharakisha kuendesha mashtaka kwa haraka bila upendeleo.[3] Idara ya usajili inahudumia ulinzi na mashtaka, inasimamia usalama, mawasiliano na kuwasaidia waathirika, mashahidi na kuweka mahabusu washukiwa.[4]

6. Uhalifu Gani Hushtakiwa Na ICC?

ICC ina uwezo kushtaki uhalifu mkuu wa aina nne:

1. **Mauaji ya Halaiki**: Inajumuisha vitendo vilivyofanyika kwa madhumuni ya kuharibu, kwa jumla ama sehemu ya makundi ya kitaifa, ukabila, rangi ama kidini, kama vile:

   (a) Kuua watu wa kundi hilo.

   (b) Kujeruhi vibaya kimwili ama kiakili watu wa kundi husika.

   (c) Kujeruhi kwa makusudi watu wa kundi husika ama sehemu yao kwa madhumuni ya kuweka majeraha ama uharibifu katika maisha yao yote.

[3] Art 43 Mkataba wa Rome
[4] Rule 13(2) RPE ICC

(d) Kuweka masharti ama hatua zenye madhumuni ya kuzuia kuzaana miongoni mwa kundi kama vile kutenganisha wanaume na wanawake ama kuua watu wenye uwezo wa kuzaa kwenye kundi hilo.

(e) Kuhamisha kwa nguvu watoto wa kundi husika kwenda katika kundi lingine.

2. **Uhalifu dhidi ya Binadamu;** Hivi ni vitendo ambavyo vinatendwa kama sehemu ya kueneza mashambuluzi ya utaratibu fulani kulenga raia na inajumuisha:

a. Mauaji.

b. Kukatisha uhai.

c. Utumwa.

d. Kuhamisha mtu ama watu kwa nguvu na bila hiari yao.

e. Kifungo au kunyimwa uhuru au ukiukaji wa sheria za kimataifa.

f. Mateso.

g. Ubakaji, utumwa kuhusiana na ngono, ukahaba wa kulazimishwa, mimba ya kulazimishwa, utoaji kizazi bila hiari ama aina nyingine yeyote ya unyanyasaji wa kimwili.

h. Ukandamizaji dhidi ya kundi lolote tajwa katika misingi ya kisiasa, rangi, utaifa, kabila, mila, dini, jinsia ama kwa misingi mingine yeyote kuhusiana na vitendo vilivyotajwa hapo juu.

i. Kutoweka kwa watu kwa kulazimishwa.

j. Uhalifu wa ubaguzi wa rangi.

k. Vitendo vingine vya ukiukaji wa ubinadamu ambavyo kwa makusudi vimesababisha mateso makubwa ama majeraha makubwa ya mwili, akili ama afya kwa ujumla.

3. **Uhalifu wa Kivita:** Ni ukiukaji wa kutisha wa haki za binadamu ambao hutokea wakati wa migogoro ya kivita. Inajumuisha vitendo ambavyo vinakiuka Mkataba wa Geneva uliopitishwa Agosti 12, 1949 na ukiukaji mwingine wa sheria za kimataifa zinazohusika na migogoro ya kivita. Iwapo ni mgogoro wa kivita ambao sio wa kimataifa, uhalifu wa kivita ikiwemo ukiukaji mkubwa wa kifungu nambari 3 cha Mkataba Mkuu wa Nne wa Geneva wa Agosti 12, 1949 na ukiukaji wa sheria na desturi kuhusiana na migogoro ya kivita ambayo sio ya kimataifa.
4. **Uhalifu wa Ukandamizaji**: Inahusu mipango, matayarisho, uanzishaji ama utekelezaji unaofanywa na mtu katika nafasi ya uongozi kuhusiana na ukandamizaji. Kitendo cha ukandamizaji kinatakiwa kihusishe ukiukaji wa Sheria ya Umoja wa Mataifa. Kitendo cha ukandamizaji kinatajwa kama matumizi ya wanajeshi kutoka taifa moja kwenda taifa jingine bila ya sababu ya msingi ya kujilinda ama kupitishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Uhalifu huu umetambuliwa hivi karibuni na bado hauwezi kushtakiwa mahakamani.

7. ICC Hupataje Kesi Zake?

Mamlaka ya ICC hupatikana katika njia tatu;[5]

(a) **Nchi mwanachama** inaweza kuwasilisha kesi mahakamani. Hata nchi ambayo sio mwanachana pia inaweza kuwasilisha kesi katika Mahakama kama uhalifu ulitendeka katika ardhi yake. Uganda na DRC zimewahi kuwasilisha kesi zao kama nchi wanachama.

(b) **Baraza la Usalama** inaweza kupeleka hali katika mahakama kwa uchunguzi. Hali ya Darfur ilipelekwa mahakamani kwa njia hii.

[5] Art 25 Mkataba wa Rome

(c) **Mwendesha Mashtaka** kulingana na mtizamo wake anaweza kuanzisha uchunguzi. Mwendesha Mashtaka anaamua iwapo mashtaka yafunguliwe kulingana na hali ilivyo, kuchunguza na kuwashtaki wahusika kwa uhalifu wa mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita. Kenya ni hali ya kwanza ambapo mwendesha mashtaka ametekeleza madaraka yake.

8. Utaratibu Wa Kesi Huwaje Katika ICC?

Mara kesi inapofikishwa mbele ya ICC kwa njia yoyote kati ya tatu zilizotajwa hapo juu, Mwendesha Mashtaka anakusanya maelezo na kuamua iwapo kuna sababu ya msingi ya kuendesha kesi hiyo. Kitengo cha kabla ya mashtaka lazima kiamue kama mwendesha mashtaka anaweza kuendelea kuendesha kesi. Hii inategemea iwapo uhalifu ulikuwa na uzito wa kutosha kwa mahakama kutimiza wajibu wake. Iwapo ushahidi utabainisha kwamba mahakama inaweza kutimiza wajibu wake, kesi inaendelea katika hatua zifuatazo;

(a) Uchunguzi.

(b) Uhakiki wa mashtaka dhidi ya watuhumiwa.

(c) Kusikilizwa kwa kesi.

(d) Hukumu na kusikilizwa kwa fidia.

(e) Rufaa.

(f) Wanawake wanaweza kushiriki katika hatua zote za kesi kama waathirika ama mashahidi. Kurasa zifuatazo zinafafanua jinsi wanavyoweza kushiriki katika uendeshaji wa kesi.

[15] Art 17(1)a Rome Statute
[16] Art 15(3) Rome Statute

SURA 2

HAKI ZA WAATHIRIKA NA ICC

Katika kesi nyingi za uhalifu, haki za washukiwa hupatiwa umuhimu. Mahakama zina madhumuni ya kuhakikisha kwamba washukiwa wanapata haki katika kesi zao. Na haki zao hazikiukwi wakati wa kukamatwa, wakati kesi inapoendeshwa, kuzuiwa mahabusu na hadi kesi inapofika tamati. ICC pia inahakikisha kwamba haki za mshukiwa zinalindwa na kutimizwa wakati wote wa kesi. Hata hivyo, tofauti na mahakama nyingine zinazoendesha kesi za uhalifu, ICC ni ya kwanza kulinda haki za waathirika bila ya kukiuka haki za mshukiwa. Mwathirika ana jukumu muhimu katika ICC.

9. Mwathirika ni Nani?

Mwathirika ni mtu aliyeteseka au kuathirika kutokana na uhalifu mkubwa ambao uko chini ya mamlaka ya mahakama. Waathirika wanaweza kuwa waliathirika moja kwa moja ama kwa njia nyingine. Waathirika wa moja kwa moja ni wale ambao waliathirika moja kwa moja au kujeruhiwa kutokana na matokeo ya uhalifu husika. Waathirika wasio wa moja kwa moja ni pamoja na wategemezi na watu wengine wa karibu

> "Waathirika wanatakiwa wahudumiwe kwa uelewa, heshima na kulinda hadhi yao. Wanayo haki ya kupatiwa muundo mwafaka wa haki na kushughulikiwa mara moja kama ilivyotajwa kwenye sheria ya kitaifa."
>
> ***Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu utaratibu wa msingi kwa Haki kwa Waathirika na Utumiaji Mbaya wa madaraka, Utaratibu namba 4***

ya familia ya mwathirika wa moja kwa moja. Aina ya uhalifu ambao ICC hushtaki washukiwa hupelekea ukiukaji wa haki ya idadi kubwa ya waathirika. Wanawake na watoto huathirika zaidi na uhalifu huu.

Haki za waathirika zinalindwa kwa njia tatu: **Kushirikishwa**, **Kulindwa** na **Fidia**.

Picha: IRIN News

10. Mwathirika Anawezaje Kushiriki?

Waathirika ambao wamenusurika katika uhalifu wa kutisha wanahamasishwa kwa mujibu wa Mkataba wa Rome kushiriki katika njia zifuatazo;

(a) Wakati wa Upelelezi

(i) Kutoa ushahidi na maelezo kwa Mwendesha Mashtaka ili aweze kupeleleza iwapo uhalifu umetendeka.

(ii) Inatakiwa aheshimiwe na asilazimishwe, kutishwa, kuteswa ama kushushwa hadhi yake.[6]

(iii) Kama atahojiwa, ahojiwe kwa lugha ambayo anaelewa. Mahakama itampatia mkalimani pale inapobidi bila gharama yeyote.[7]

(iv) Kuhojiwa huku mwanasheria akiwepo.[8]

[6] Art 55 Mkataba wa Rome
[7] Art 55 Mkataba wa Rome
[8] Art 55 Mkataba wa Rome

Ili kuweza kushiriki katika awamu ya upelelezi, mwathirika, familia yake ama wategemezi wa mwathirika wa moja kwa moja, wanatakiwa watoe ushahidi wa kutosha ili kuonyesha kwamba kuna sababu za msingi kuamini kwamba waathirika waliathiriwa kutokana na matokeo ya uhalifu uliotendeka ndani ya uwezo wa mahakama.

(b) Wakati wa kusikilizwa kesi

Waathirika na mashahidi wanaweza:

- Kutoa ushahidi iwapo wataitwa kama mashahidi wa upande wowote kesi inaposikilizwa.
- Kutoa maoni yao katika hatua yeyote wakati kesi ikiendelea kusikilizwa, hukumu na rufaa. Hii inapatia nafasi mahakama kupata maoni na kupata maelezo halisi kuhusiana na uhalifu uliodaiwa kutendwa.
- Kuwa na haki ya kuchagua mwakilishi wa kisheria. Mwakilishi wa kisheria ni wakili ambaye ni mtaalam katika sheria ya uhalifu wa kimataifa na taratibu za kesi hizo. Ambapo mwathirika ama kundi la waathirika hawawezi kumudu mwakilishi wa kisheria, ICC itatoa msaada wa kifedha.[9]
- Kupatiwa taarifa kuhusu jinsi kesi inavyoendelea na uamuzi wa mahakama. [10]

11. Je Waathirika Wote Wanaweza Kushiriki?

Sio waathirika wote wanaweza kushiriki katika kesi kwa sababu mahakama italemewa na idadi kubwa ya watu. Mara mwathirika anapowasilisha maombi ya kushiriki, majaji husika wanaangalia kama

[9] Sheria 90 RPE
[10] Sheria 92 RPE

mtu huyo aliathirika na wanaamua lini na jinsi mwathirika anaweza kushiriki katika kesi. Vigezo ambavyo mahakama imeweka ili kuweza kuwa mwathirika ni:[11]

i. Mwathirika anatakiwa awe na asili ya sehemu aliyotoka;

ii. Mwathirika lazima awe amepata madhara

iii. Uhalifu ambao madhara yametokea lazima uwe chini ya uwezo wa Mahakama;

iv. Kunatakiwa kuwe na ushahidi kwamba madhara aliyopata mwathirika yalitokana na uhalifu ambao mshukiwa anashtakiwa nao.

12. Mwathirika Anawezaje Kuomba Kushiriki?

Waathirika wanaweza kuomba kushiriki kwa kutumia fomu wanayowasilisha katika idara ya Ushiriki na Fidia ya Waathirika (VPRS) ya Mahakama.

Ulinzi wa Waathirika

ICC inalo jukumu la kuwalinda waathirika na mashahidi. Inatambua kwamba wanaweza kuwa wameathirika kisaikolojia na huenda wakawa bado wako chini ya tisho la kulipiza kisasi kwa kuchukua hatua ya kujitokeza na kutoa ushahidi. Ulinzi unaotolewa kwa waathirika unahusika na usalama wao, hali njema ya mwili na akili, heshima na faragha. Mahakama inajali umri, jinsia, afya na aina ya uhalifu. Kwa mfano, wakati uhalifu unapohusu ukandamizaji wa kingono ama jinsia dhidi ya watoto, hatua maalum zitachukuliwa kulingana na mahitaji ya waathirika.

[11] Msingi wa kukubalika kuwa mwathirika ulitajwa katika kesi ya Lubaga

13. Je, Waathirika Na Mashahidi Wanalindwaje?

Waathirika:

i. Wanapatiwa ushauri nasaha na matibabu mwafaka katika chumba cha mahakama ikiwemo kuhakikisha kwamba hawaonekani na mshukiwa pale inapobidi.

ii. Waatalam wa masuala ya madhara ya kisaikolojia wanapatikana ili kuwahudumia waathirika.

iii. Mashahidi wanayo haki ya kuwa na mtu wa familia pamoja nao wakati wanapotoa ushahidi.

iv. Majaji wanahakikisha kwamba hawanyanyaswi ama kutishwa wakati wa kuhoji.

v. Faragha yao huheshimiwa na kitengo cha kabla ya mashtaka na kitengo cha kuendesha kesi ambapo kama ni muhimu italinda waathirika na mashahidi kutoka vyombo vya habari. Mahakama pia inaweza kuchukua ushahidi wa waathirika ama mashahidi kwa njia ya video ama njia nyingine za elektroniki au njia maalumu.[12]

[12] Art 68(2) Mkataba wa Rome

FIDIA

14. Fidia ni nini?

Mkataba wa Rome unatoa nafasi ya fidia kwa waathirika wa uhalifu wa kutisha. Fidia hii hupatiwa waathirika kwa majeraha waliyopata. Fidia hii sio pesa pekee bali inajumuisha njia nyingine ambazo zinatambua athari kwa mwathirika. ICC inaamua uzito wa athari, hasara ama majeraha kwa mwathirika na kutoa nafasi ya fidia. [13]

15. Kuna Aina Ngapi Za Fidia?

Fidia zinaweza kutolewa kwa njia tatu:

Kurudisha hali ya awali
Ni njia inayotumika kurudisha hali ya awali ya mtu ambayo angekuwa kama kusingetokea uhalifu husika. Inaweza kujumuisha kurudisha mali ambayo ilichukuliwa.

Fidia
Hizi ni pesa zinazolipwa kama malipo kwa majeraha ama makosa ambayo mtu alitendewa.

Marekebisho ya kisaikolojia
Ni hali ya kumrudisha mtu katika hali ya kawaida katika jamii. Watu huathirika kisaikolojia na kupoteza nafasi zao katika jamii kutokana na uhalifu. Marekebisho hutoa mfumo wa usaidizi kusaidia watu kurudi katika nafasi zao sahihi katika jamii.

[13] Art 75(1) Mkataba wa Rome

16. Utaratibu Gani Hufuatwa Katika Kuomba Fidia?

Maombi ya fidia yanatakiwa yafanywe kwa maandishi na yaambatanishwe na maelezo yafuatayo;

i. Utambulisho na anuani ya mtu anayewasilisha ombi la fidia

ii. Maelezo ya majeraha ama hasara iliyotokea kwa mfano: uharibifu wa mali ama athari ya kiakili

iii. Mahali na tarehe ya tukio lililosababisha hasara ama majeraha.

iv. Wakati fidia ya mali inapotakiwa, maelezo ya mali kama vile, iwapo ni nyumba ya chumba kimoja cha kulala, yenye vitu ndani. Madai ya fidia.

v. Madai ya marekebisho ama aina nyingine ya suluhisho.

vi. Nyaraka husika zinazoambatanishwa kama vile: hati ya kumiliki ardhi na majina na anuani ya mashahidi.

Kesi za fidia zitachapishwa ili waathirika wengine wajue. Malipo ya fidia yanaweza kufanyika katika njia mbili. Mtuhumiwa aliyepatikana na hatia atatakiwa alipe fidia ama inaweza kuamriwa fidia ilipwe katika Hazina ya Umma. Pesa ambazo ICC inapokea kama malipo ya faini ama mali iliyosalimishwa inalipwa katika Hazina ya Umma ambayo imeundwa kwa manufaa ya waathirika.[14] Iwapo waathirika ni wengi, fidia zinatolewa kupitia Hazina ya Umma na inaweza kulipwa kupitia Serikali husika, mashirika ya kitaifa na kimataifa.[15]

[14] Art 79 Mkataba Rome
[15] Rule 98 RPE

17. JE KUNA IDARA MAALUM KATIKA ICC AMBAZO HUSAIDIA WAATHIRIKA?

Ili kusaidia waathirika, Mahakama imeunda vitengo viwili maalum;

1. **Kitengo cha Ushiriki na Fidia kwa Waathirika (V.P.R.S)-**

   Jukumu lake kuu ni pamoja na kuwasaidia waathirika kujaza maombi na kushiriki katika kuomba fidia. Kitengo hiki pia husaidia waathirika kupata ushauri wa kisheria na kuwakilishwa. Pia kina madhumuni ya kuendeleza na kulinda uhusiano na waathirika na makundi mengine, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na kutoa maelezo ya utaratibu wa kudai fidia.

2. **Kitengo cha Waathirika na Mashahidi (VWU)**

   ICC inatambua kwamba waathirika wamenusurika na pia wanaweza bado kuwa hatarini kulipiziwa kisasi kama watatoa ushahidi. VWU iliundwa ili kuwalinda waathirika katika muda mfupi na muda mrefu. Hatua hizo zinahusiana na utaratibu wa ulinzi, kutoa nafasi ya kuingilia panapokuwa na mgogoro, kutoa maelezo kabla na baada ya ushahidi kutolewa, kupatikana kwa huduma ya matibabu, ushauri nasaha na usaidizi mwingine kwa waathirika na mashahidi wanaoshiriki katika kesi.

   Kitengo hiki kinashirikiana na idara nyingine za mahakama kwa kutoa mafunzo na kuhakikisha mahitaji maalum ya watoto, walemavu, waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia na wazee wanalindwa. Mahitaji ya kimila, kidini na kijamii ya waathirika pia yanatiliwa maanani wakati hatua za usalama zinapochukuliwa. Kitengo hiki pia kina utaratibu wa kulinda mashahidi ili kulinda faragha yao, siri na usalama wa waathirika, mashahidi, familia zao na kujumuisha kuwapatia makazi sehemu nyingine pale

inapobidi**.** Kinashirikiana na nchi shirika ili kuhakikisha ufanisi wa kuwapatia makazi mapya waathirika na mashahidi ambao wanafika mbele ya mahakama.

Huduma za VWU zinatolewa katika pande zote za kuendesha mashtaka na utetezi katika njia iliyo sawa na inapatikana katika hatua zote wakati kesi inapoendelea kusikilizwa. Mwathirika na shahidi anaweza aidha kuomba usaidizi ama idara za mahakama zinaweza kuwaelekeza kwenye idara hiyo.

SURA 3

WANAWAKE NA ICC

Wanawake wana haki zote za waathirika ambazo hutolewa na ICC. ICC pia inatambua haki maalum za wanawake kwa sababu ya athari kubwa ya uhalifu dhidi yao. Wanawake huathirika na uhalifu wote ambao uko chini ya ICC ambao ni mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu, uhalifu wa kivita na uhalifu wa ukandamizaji.

18. Uhalifu Gani Hutendwa Dhidi Ya Wanawake?

Nchini Kenya wakati wa vurugu za baada ya uchaguzi, wanawake na watoto waliathirika vibaya na mambo ambayo yametambuliwa

kwamba ni uhalifu dhidi ya binadamu. Ni pamoja na mauaji, unyanyasaji wa kingono, kukatwa viungo vya mwili, kubakwa na makundi ya watu, mateso ya mwili, uharibifu wa mali, kupoteza ardhi, ukosefu wa chakula, kuteketezwa kwa mali, kutekwa nyara, kuvamiwa, kuhamishwa kwa nguvu, kubeba mimba kwa lazima na ukahaba.

Wahusika wengi walikuwa ni maafisa wa usalama na wanaume katika jamii husika ambao walitumia nafasi ya vurugu zilizokuwepo. Uhalifu huu ulisababisha vifo, ulemavu, mateso ya kiakili na matokeo yake yalikuwa kuundwa kwa makazi ya wakimbizi wa ndani ya nchi. Baadhi ya uhalifu hufanywa dhidi ya wanawake peke yake kwa sababu ni wanawake ambao kwa mfano, hubebeshwa mimba kwa nguvu.

"Wanaume wengine walikuwa wanawakimbiza watu barabarani. Nilikimbia na watoto wangu. Niliona mwanaume akiuawa kwa kukatwa na panga na kupigwa marungu wakati nilikuwa nakimbia. Nikiendelea kukimbia, nilijikwaa na kuanguka karibu na mto katika shule ya msingi ya Kipkendui. Mwanangu kitinda mimba alianguka mbali nami na aliumia na kulia. Watu wengine walikuwa wananikimbiza na nilipoanguka, wanaume wawili walinikamata. Walirarua chupi yangu na wote wakanibaka kwa zamu…"

Shahidi wa IDP anayeishi uwanja wa maonyesho wa Eldoret aliwaeleza wachunguzi wa CIPEV.

Hata wakati uhalifu kama ubakaji unapotendeka dhidi ya wanaume pia, wengi wa waathirika ni wanawake. Kwa hiyo ICC imejumuisha uhalifu unaoathiri wanawake hasa kulingana na Mkataba wa Rome.

19. Mahakama Huwalindaje Wanawake?

Changamoto kubwa katika kuwashtaki washukiwa wanaotuhumiwa kuhusika na uhalifu dhidi ya wanawake ni kwamba waathirika wengi wanawake hawajitokezi kutoa ushahidi. Ili kuhamasisha wanawake kutoa ushahidi na kuondoa woga na hofu zao, ICC inaweza kusikiliza kesi katika kamera (kwa faragha) ikiwa ni hatua ya kuwalinda waathirika.

> …. Nilienda nyumbani kwangu. GSU walinifuata na kusema wanatafuta vijana ambao walihusika na vurugu. Wanaume watatu maafisa wa GSU waliingia nyumbani kwangu. Sikufunga mlango na walipoingia sikujali kufunga sababu walikuwa maafisa wa usalama ambao wanatakiwa watulinde. Afisa mmoja wa GSU alisimama mlangoni wakati wengine wawili walipoingia ndani…Afisa mmoja wa GSU alinishika na kusema, "hatuwezi kukuacha." Alinitupa kitandani na kunipiga usoni. Alirarua chupi yangu na kunibaka. Halafu wa pili akanibaka….Ilisumuliwa kwa CIPEV na mwanamke wa umri wa miaka 55 kutoka Kibera. (CIPEV katika 255)

Wakati wa upelelezi, wapelelezi wanatakiwa wakusanye ushahidi kutoka kwa wanawake kwa jinsi ambayo itajali maslahi yao na kwa ufanisi. Mwendesha Mashtaka anahitajika ateue mshauri kuhusiana na vurugu za unyanyasaji wa jinsia na ngono na kushauri jinsi suala hili linavyoshughulikuwa na watu walioathirika.

Utaratibu wa ICC na sheria zilizopo zinajali hali ya wanawake na madhumuni yake sio kuwaongezea shinikizo wakati wa kesi. Kwa mfano maana ya ubakaji katika Mkataba wa Rome unatambua kwamba kimya cha waathirika wakati wa uhalifu wa unyanyasaji wa kingono hauwezi kutambulika kwamba walikubali kutendewa hivyo. Ushahidi wa tabia ya masuala ya mapenzi ya mwathirika kabla tukio ama mara baada ya kitendo cha ngono haukubaliki, ushahidi wa mwathirika hauhitaji kulinganishwa na ushahidi mwingine ili ukubalike.

20. Wanawake Wana Jukumu Gani Lingine Katika ICC?

Ajira

Wanawake wameajiriwa katika ICC kama wafanyakazi wakiwemo pia majaji. Mwendesha Mashtaka na Msajili huajiri wafanyakazi kulingana na haja ya uwakilishi wa haki wa jinsia. Mbali ya kuhitaji utaalam katika kazi husika kama vile Sheria ya kimataifa ya haki ya binadamu, pia kuna haja ya wafanyakazi kuwa na utaalam juu ya uhalifu dhidi ya wanawake.

Huduma za nje

ICC ina mpango wa huduma ya nje ya mahakama ambao uliundwa ili kuhakikisha jamii zilizoathirika kwenye migogoro kwenye nchi iliyo katika hali ya uchunguzi kama vile Kenya, zinaweza kuelewa na kufuatilia kazi ya mahakama kupitia hatua mbalimbali za shughuli zake. Kupitia mpango huu, mahakama inawasiliana na jamii zilizoathirika, kuelewesha na kusaidia uendeshaji wa shughuli za mahakama, kufanya mikutano na makundi yaliyolengwa kama vile wanawake na kutumia radio na vyombo vingine vya habari kufikia idadi kubwa ya wananchi.

Katika hali ya Kenya, mpango wa mahakama za nje zinafanywa ili kuelewesha utaratibu wa uendeshaji wa Mahakama miongoni mwa wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa, makundi ya wanawake, waandishi wa habari, viongozi na wawakilishi wa jamii zilizoathirika. Kwa hivyo wanawake wanaweza kuhamasishwa ili kuelewa kinachoendelea katika ICC na jinsi inavyowahusu pia.

HITIMISHO

Vurugu za baada ya uchaguzi za mwaka 2007 hadi 2008 zimekuwa ni chanzo cha upelelezi katika ICC kwa sababu ya uwezekano wa kutendeka uhalifu dhidi ya binadamu. Wanawake waliathirika zaidi na vurugu hizo, hivyo ni muhimu waelewe ICC ni nini na jinsi wanavyoweza kushiriki katika kupata haki Mahakamani.

Madhumuni ya chapisho hili ni kuelewesha kuhusu mfumo na kazi ya Mahakama, makosa ambayo hushtakiwa nayo na haki za waathirika na hasa za wanawake. ICC ni Mahakama ya kwanza kimataifa kumshirikisha kwa kiasi kikubwa mwathirika. Imelenga zaidi kwa mwathirika na pia wanawake.

Wanawake wa Kenya kwa binafsi na pia kwa pamoja wanatakiwa kutumia kila nafasi kushiriki kwenye ICC na kuchangia kukomesha kutoshughulikiwa kwa uhalifu hatari Kenya. Wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia utaratibu wa mahakama kushiriki katika kila hatua ya kesi, kutafuta fidia na kushiriki kwenye mpango wa nje ya mahakama. Inatarajiwa kwamba kushtakiwa kwa wale waliohusika zaidi na uhalifu kutazuia uhalifu kama huu kutokea tena Kenya katika siku zijazo.

Notes

FRIENDS OF FIDA APPLICATION FORM

Name of Friend _____

Please tick appropriate title:

Corporate Body	Organisation	Individual

Details of Applicant

ORGANISATION OR CORPORATE BODY

Contact person		Mobile
Telephone	Code	City
Mailing address		
E-mail		Fax
Physical address		
Road/Street	Building	Floor
Email		Fax

INDIVIDUAL

Male	Female
ID/PP/DL. No.	Occupation
Telephone	Mobile
E-mail	Fax
Mailing address	Code

CATEGORY	KSHS/YEAR	COLOUR CODE
Lifetime friend	100,000 and above	Gold
Sustainer Friend	51,000 – 100,000	Silver
Committed Friend	10,100 – 50,000	Copper
True Friend	5,100 – 10,000	Blue
Supportive Friend	2,100 – 5,000	Green
Loyal Friend	1,000 – 2,000	Red

Introduced to Friends of FIDA by _____

Kindly send your contributions to FIDA-Kenya, alternatively you can deposit your cheque/cash payment to our Account Number 0103007038 at Citibank and forward the banking slip to us for receipting and acknowledgement purposes.

I enclose herewith cheque/cash to the value of _____ For the Year _____

Signature _____ Date _____ Received by _____ Date _____

Notes